JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

DODOMA

.1

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI

Namba za Simu

Mkuu wa Shule 0762773954/0627812420

Makamu Mkuu wa Shule 0625430592/0759505720/0766979430

Matron 0748246525

Patron 0753198085

Shule ya Sekondari Mizengo Pinda

S.L.P 607

Tarehe……………………….

Mzazi/Mtezi wa Mwanafunzi…………

S.L. P…………………………………..

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MIZENGO PINDA HALMASHAURI YA MPIMBWE MKOA WA KATAVI MWAKA……………………………………………..

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka wa masomo………………….. Tahasusi ya………………… Shule ya sekondari Mizengo Pinda ni ya bweni na ni ya wavulana na wasichana. Shule ipo umbali wa kilomita 110 Kusini Magharibi mwa mji wa Mpanda.

Shule iko karibu na CHUO KIKUU CHA KILIMO CHA SOKOINE (SUA) CAMPUS YA MIZENGO PINDA kilichopo Mkoa wa Katavi. Usafiri wa basi kutoka Mjini Mpanda unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda, nauli ni shilingi elfu kumi na mbili (TSh 12000/=).

Kwa wanaotokea Dar es salaam wanaweza kupitia Mbeya au Tabora- Kwa watakaopitia Mbeya watapanda gari la kwenda Sumbawanga na wakifika Sumbawanga wetapanda gari linalokwenda Majimoto au watapanda gari la kutoka Mbeya Kwenda majimoto na kushuka kituo cha mabasi cha Kibaoni na kwa watakaopita Tabora watapanda gari la kwenda Sumbawanga na kushuka kituo cha mabasi Kibaoni au wanaweza kupanda gari la kwenda Mpanda wakifika Mpanda watapanda gari la kwenda Majimoto na kushuka Kibaoni.

Kwa wanaotokea mikoa ya kaskazini kama Vile Kilimanjaro, Arusha, Manyara na maeneo mengine watapanda gari linalokwenda Mpanda kwa kupitia Mkoa wa Tabora na kushuka Mpanda mjini,Usafiri wa basi kutoka Mpanda Mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda, nauli ni shilingi elfu kumi na mbili (TSh.12000/=) panda mabasi ya kwenda Majimoto na kushuka Kibaoni au wakifika Tabora watapanda gari tinalokwenda Sumbawanga na kushuka Kituo cha mabasi Kibaoni Kilichopo umbali wa mita 700 kutoka Shuleni. Kutoka Kibaoni utachukua pikipiki (bodaboda) moja kwa moja hadi shuleni nauli yake ni Shilingi elfu moja (TSh 1,000) tu au waweza kuja kwa miguu hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………………, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe…………………..Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………………….

1. Mambo muhimu ya kuzingatia:

1.1 Sare za Shule

i. Sare ya Shule hii ni: -

KWA WASICHANA: Sketi 2 (moja iwe rangi ya orange(karoti) na nyingine iwe rangi ya ugolo kitambaa Esteem original no 1, iwe ya linda box, linda 8. linda moja kubwa mbele na nyuma na matatu upande wa kulia na matatu upande Wa kushoto. (SKETI ZIWE NDEFU SANA ZIFIKE KWENYE KIWIKO CHA MIGUU. SKETI FUPI HAZITAKIWI KABISA)

KWA WAVULANA: Suruali 2 za rangi ya ugolo kitambaa Esteem original no 1, zinazotosha kiuno zenye marinda mawili (SURUALI ZENYE MSHONO WA MODO HAZITAKIWI KABISA PIA SURUALI FUPI HAZIRUHUSIWI)

ii. Mashati mawiti meupe yenye mikono mirefu na yasiyo na urembo wowote.

iii. Kwa watakao vaa hijabu, ni Majuba mawili ya rangi nyeupe yawe marefu yafunike kifua cha Mwanafunzi, pia yawe marefu kufunika Kifundo cha Mikono akisimama yasiguse Kiuno. Pia, Majuba mawili ya rangi ya bluu Bahari kwa ajili ya kushindia. Rangi nyingine hazitakiwi.
iv. Sare za michezo kwa Shule hii ni
   - Track suit ya rangi Dark blue yenye mistari ya rangi nyeupe pembeni kwa wavulana,
   - Track suit ya rangi ya kijivu mistari ya rangi nyeupe pembeni kwa wasichana
   - T-shirt ya pinki na Bukta ya pinki kwa wasichana
   - T-shirt ya ugolo na bukta ya ugolo kwa wavulana
   - Viatu vya michezo (raba), Kwa wavulana na wasichana
v. Viatu pair mbili vya shule ni vyeusi visiwe vya kufunga na Kamba na viwe na visigino vifupi.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta moja lenye nembo ya shule.
ix. Nguo za kushindia (shamba dress)
   - Suruali nyeusi ya kitambaa kwa wavulana
   - Sketi kitambaa cha draft ndogo (kimasai) ya rangi ya orange(karoti) mshono wa solo ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu kwa wasichana.
x. Tai
   - tai mbili rangi ya ugolo kwa wavulana
   - tai ya ugolo moja na orange 1 kwa wasichana
xi. Tisheti (T-shirt) mbili zenye nembo ya shule.

NB: Ili kuepuka usumbufu wa kukosea na kushona mara mbili, ukiona ugumu aje ashone kwa mafundi walioko shuleni.

Mahitajj mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kujanayo shuleni

i. Unatakiwa kuja na daftari kumi (10) aina ya Counterbook Quire 3 nakuendelea.
ii. Ream
   -A4 Mbili (2) kwa mwaka **(kwa wavulana)**
   **-**A3 moja (1) kwa mwaka **(kwa wasichana)**
iii. Godoro la sponji futi mbili na nusu kwa sita
iv. Mashuka dozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua rangi nyeupe
v. Nguo za ndani za kutosha:

vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli. kijiko na kikombe):
vii. Ndoo 3 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
viii. Kwanja 1 (wavulana). jembe 1lenye mpini (Wavulana, Wasichana), reki 1 (wasichana),
ix. mfagio mrefu wa kutolea buibui 1 (Wavulana ), hardbrush 1 (wavulana), toilet scrubing brush1 (Wasichana), squizer 1 na ndoo yake (Wasichana), mfagio wa nje (Wasichana, Wavulana)
x. taa ndogo za sola kwa matumizi yake mwenyewe pale umeme unapokatika.
xi. Sabuni ya maji kwaajili ya kusafishia chooni lita5 na lita moja ya ARO (dawa ya kusafishia masink ya chooni)

### 1.2 Michango mbalimbali

**a. Shuleza Bweni**

| Na | Aina a Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendesha'i wa Shule | 65,000/- |
| 3. | Tahadhari | 5,000/- |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Michango yote ya fedha iingizwe katika akaunti ya Shule iliyopo katika Benki ya NMB Account No 61901200077 inayoitwa MIZENGO PINDA SEC CAPITATION ACC, kisha tuletee Bank pay—in-slip ukiwa umeandika jina lako na mchanganuo wa malipo nyuma ya karatasi hiyo.

Kwa mwanafunzi asiye na bima ya afya,akatiwe bima ya afya au aje na Tsh.50400/=(cash)kwaajili ya kumkatia bima ya afya ili kuepuka usumbufu pindi mwanafunzi atakapougua

### 2.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

- Shule inaendeshwa kwa mujibu Wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu. Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukUmU la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini, Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakafa yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi. wazazi, wafanyakazi wote. wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za Shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shute na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya Shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi Wako katika Shule hii,
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingfra ya shule;
vii. Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwe;
viii. Kuzingatja ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni-

**32 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na**:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, waljmu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzj kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo unaokubalika;
vii. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
viii. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
ix. Kufuga ndevu;

x. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
xi. Uvutaji wa sigara;
xii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xiii. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xiv. Kusababisha mimba,
xv. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xvi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xvii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xviii. Kudharau Bendera ya Taifa,
xix. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xx. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**MUHIMU;**

+ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

+ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbanl kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA
SEKONDARI MIZENGO PINDA

Saini ya Mkuu wa Shule ..........................................................

Jina la Mkuu wa Shule ALICKO J KAMINYOGE

..........................................................

Mhuri wa Mkuu wa Shule .

NB: Kwa siku za hivi karibunj kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama wafimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE. NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: •

- ➢Mkuu wa shule 0762773954/0627812420
- ➢ Makamu Mkuu wa Shule 0625430592/0759505720/0766979430
- > Mwandamizi Taaluma 0766647159

KIAMBATA 'A'

ORODHA YA VITABU WA MASOMO WANAVYOTAKIWA KUNUNUA WAZAZI Kwa sababu Shule hii ina uhaba wa vitabu, ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:-

A) HISTORIA: -

12. History for Secondary Schools Form five (Tanzania Institute of Education)
13. History for Secondary Schools Form Six (Tanzania Institute of Education)
14. History for secondary schools: Form Five (TIE).
15. History for Secondary Schools: Form Six (TIE)

b) VITABUWA KISWAHILI: -

4. Kltangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu. Wandishi: - H.J.M. Mwansoko,

5. Kiswahili Sekondari — Kidato cha Tano (Tl E)
6. Kiswahili Sekondari Kidato cha Sita (TIE)

7. VITABUVYAUCHAMBUZI USHAIRI

- Fumbo linaloelea Nyambali C. M. Nyangwine
- Andamo msafiri safarini Muhamed K. Nghasani
- Malenga wa ziwa kuu Wallah bin Wallah

Wosi awa baba Ahmed M. Amanzi

RIWAYA.

- Dunia uwanja wa fujo E. kezilahabi
- Ua la faraja W.E. Mkufya
- Mirathi ya hatari C.G. Mng’ong’o
- Wasifu wa Siti binti Saad Shaaban Robert

TAMTHILIYA

Mkwava wa uhehe M.M. Mulokozi
Shuja Mirambo E. Mbogo
Usaliti mjini F. Ibuga

C) VITABUVYA JIOGRAFIA

Geography for secondary school form five and six (TIE)

D) FASIHI YA KISWAHILI

Fasihi ya Kiswahili, kitabu cha mwanafunzi; kidato cha tano. (TET)

E) ACADEMIC COMUNICATION

Academic Communication for advanced Secondary Schools Student's Book Form five (TIE)

F) LITERATURE IN ENGLISHI

Literature in English forb Advanced Secondary Schools Student's Book; Form five (TIE)

G) VITABU WA LANGUAGE

English Language for Secondary Schools; Form five (TIE)

**LIST OF NOVELS.**

a) Owels,G.(2024). **Animal Farm**. East African Educational Publishers Ltd.
b) Wakemanlin,J.(2024). **Chasing the Leopard Finding the Lion** .Mkuki na Nyota Ltd.
c) Nyangwine, N.C.M. (2023). **The Opportunist Elite**. Mbesa Books Distributors.
d) Mwaisekla,F. (2011). **The Horizon Unveiled**.fgd Tanzania Ltd

**LIST OF PLAYS**

i. Topan,F.(2023). **A Taste of Heaven**.Mkuki na Nyota Lublishers.
ii. Ibsen,H.(2023). **An Enemy of the People**.East African Educational Publishers Ltd.
iii. gogol,n.v.(2024). **The Government Inspector**. East African Educational Publishers Ltd.

**LIST OF POETRY**

a. Mabala et al. (2023). **Summons:Poems from Tanzania**.Mkuki na Nyota Publishers Ltd.
b. Angira, J. (2024). **Poets of Africa**. East African Educational Publishers Ltd.
c. **Lament of silent & other poems**. East African Educational Publishers Ltd.

E) HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

Historia ya Tanzania na Maadili kitabu cha mwanafunzi; kidato cha tano(TET)

KIAMBATA **B**

Picha ya mwanafunzi

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE
NA NAFASI YA SHULEAUYOPEWA

A. TAARIFA 31 NAFSI YA MWAÑAFUNZI (ljazwe namwana

1 ,Jinakamililamwanafunzi
2 Tahasusi Jinsia (Me/ Ke) Uraia…………
3 Kabila / msikiti anakosali ni……………………
4 Tarehe ya kuzaliwa……………………………..
5 Mahali alipozaliwa Kitongoji/ mtaa……………………………

Kijiji ____________ Kata ____________________ Tarafa ____________________ Wilaya/Mji____________________
Mkoa____________________
6. Yatima / Sio yatima ____________________ ______________________ Amempoteza



B, KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA

MİMİ KIDATO CHA MWAKA MCHEPUO …………Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yoîe. Hivyo nakubali kuipokea/ sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubalj kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimişhwa, Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.

TAREHE:………………………………… SANI: ……………

C.KUKUBALI SHERIA NA KANUNI ZA SHULE:

MWANAFUNZI:

Mımi……………………………………wa Tahasusi ya…………………………nimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomü hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course, Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti. sheriaj kanuni, tarallbu, miangozo ya shule na maelekezo mengine

nitakayopewa na walimu watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shula Sitashirjki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zjlizoorodheshwa kwa kila kosa Tarehe.......................Saini ..................

D.TAARIFA YA MZAZI/MLEZI ANDIKA MAJINA MATATU)

1. JINA LA BABA......................................

| |
|---|
| Richa ya baba |

MAHALI ANAPOISHI.........................................................................

KITONGOJI...................KIJIJI:.......................KATA:...............................

TARAFA........................................ KAZI YA BABA.............................. NAMBA YA SIMU YA BABA................................................................ S. L. P.................................. MJI.............................................................................

2 JINA LA MAMA.........................................................

| |
|---|
| Picha ya Mama |

JE, MAMA YAKO AMEFARIKI?..................... MAHALI ANAPOISHI...............................................

KITONGOJI...................................... KIJIJI.......................... KATA....................

TARAFA...................................NAMBA YA SIMU YA MAMA...........................

S. L. P ................................ MJI.........................................................................

ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI (AJAZE SEHEMU HII)

| |
|---|
| Picha ya m/ezi wa küme |

3.JINA LA MLEZI WA KIUME...

MAHALI ANAPOISHI...............................................UHUSIANO.................

SIMU.................................. S. L. P........................ MJI..............................

KAZI ANAYOFANYA.......................................... MWAJIRI.......................

4.JINA LA MLEZI WA KIKE…....................................................................

| |
|---|
| Picha ya m/ezi wa kike |

MAHALI ANAPOISHI. ………………. UHUSIANO..................

SIMU.........................................S. L. P……MJI ..............................KAZI ANAYOFANYA.......................................MWAJIRI...............

E. MZAZI/MLEZI (Azaje Sehemu Hii):

Mimi............................................... nikiwa Mzazi/Mtezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi________________________ na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa:

kumshaurl ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu rnzuri, Pia naahidi kulipa ada ya shute na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shute Nitahudhuria vikao vya shute kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubatiana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo. TAREHE: ………… SAINI………………………………

F: SEHEMU YA NDUGUWAKARIBU:

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi anapokuwa shuleni. Majina matatu mfano: ROSE ZABRON MUSSA.

| JINA | UHUSIANO | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|
| 1. ………………………………………… | ………………………… | ………………………………… |
| 2. ………………………………………… | ………………………… | ………………………………… |
| 3 ………………………………………… | ………………………… | ………………………………… |
| 4.………………………………………… | ………………………… | ………………………………… |

KIAMBATA 'C'

THE REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MPIMBWE DISTRICT COUNCIL

PART A

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO: Medical Officer FROM: THE HEADMASTER

MIZENGO PINDASECONDARY SCHOOL.

Po BOX 607

MPANDA-KATAVI

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time academic study.

A: 1. (a) Eye —sight (b) Hearing (c) Speech (d) Veneral Disease (e) Leprosy (f)

Limbs (g) Epilepsy

2. Neuroses
3. Other serious diseases B: BLOOD GROUP

______

PART: B FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above-named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for e full time academic studies at your school, (a) Eyesight.................................................................................

(b) Hearing...............................................................................

(c) Speech..................................................................................

(d) Veneral disease...........................................................

(e) (e) Leprosy...........................................................

(f) Limbs ..........................................

(g) Epitepsy.......................................................

(h)Neurosjs.............................................................

(i) Pregnancy..................................................

(j) Other serious diseases..........................................................

(k) BLOOD GROUP......................................

DATE..........SIGNATURE........................ ... OFFICIAL STAMP-.-.-.........................

**BAADHI YA VIFAA VINAVYO PATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE NA BEI ZAKE.**

## 1. STATIONARY

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | RIM PAPER (A4) | TSH. 15,000/= |
| 2. | COUNTER BOOK QUIRE 2 | TSH. 2,500/= |
| 3. | COUNTER BOOK QUIRE 3 | TSH. 3,500/= |
| 4. | COUNTER BOOK QUIRE 4 | TSH. 4,500/= |
| 5. | SCIENTIFIC CALCULATOR | TSH. 40,000/= |
| 6. | DAFTARI ZA MSOMI | TSH. 1,000/= |
| 7. | PENI | TSH. 200/= |
| 8. | MKEBE (MATHEMATICAL SET) | TSHS. 2,500/= |

## 2. VIFAA VYA USAFI

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | JEMBE NA MPINI | TSH. 7,000/= |
| 2. | BRUSH NGUMU | TSH. 3,000/= |
| 3. | BRUSH LAINI (SOFT BROOM) | TSH. 3,000/= |
| 4. | SQUIZER NA NDOO YAKE | TSH. 10,000/= |
| 5. | NDOO NDOGO LITA 10 | TSH. 5,000/= |
| 6. | FAGIO ZA CHELEWA | TSH. 2,000/= |
| 7. | BESENI LA KUFULIA NGUO | TSH. 4,000/= |

## 3. NGUO

| S/NO | NGUO | BEI |
|---|---|---|
| 1. | SHATI TOMATO | TSH. 10,000/= |
| 2. | SHUKA NYEPESI KIJANI KIBICHI | TSH. 12,000/= |
| 3. | NETI | TSH. 8,000/= |
| 4. | VIATU (SIMPLE ZA BILA KAMBA) | TSH. 12,000/= |
| 5. | NGUO ZINGINE MUHIMU ZINAPATIKANA | - |
| 6. | TRACK SUIT | 22000/= |

## 4. VYOMBO VYA CHAKULA

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | SAHANI ZENYE MFUNIKO | THS. 3,000/= |
| 2. | VIKOMBE | TSHS 1,000/= |
| 3. | KIJIKO | TSHS. 500/= |

## 5. GODORO………………………………………………………………………….TSHS. 40,000/=

**6. SARE ZA SHULE**

1. BLAUZI YA KUSHINDIA



**2.SKETI YA UGOLO-(** Esteem original no 1**)**



**3.SURUALI YA UGOLO (**Esteem original no 1**)**



**4.SKETI YA ORANGE(**Esteem original no 1**)**



**5.SHAMBA DRESSS (WASICHANA)**



**6.SHAMBA DRESS- SURUALI NYEUSI (**Esteem original no 1**)(WAVULANA)**



**7. TRACK SUIT YA KIJIVU (WASICHANA)**



**8. TRACK SUIT -DARK BLUE(WAVULANA)**

